# NGAO YA SARUFI

## MITIHANI YA SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (NA MAJIBU)

**VIPENGELE ANUWAI VYA SARUFI YA SEKONDARI VIMETAHINIWA**

NA

**MWALIMU ONYANGO, DIRA SERIES.**

(TABARUKU KWA WATAHINIWA WA 2021)

TOLEO LA KWANZA, 2021

# MTIHANI WA KWANZA

a) Andika sifa **mbili mbili** bainifu za sauti zifuatazo ( alama 2)

i) /gh/

ii) /b/

bi)Eleza maana ya sauti mwambatano ( alama 1)

ii)Taja silabi **mbili** mwambatano za mdomoni ( alama 1)

c)Ainisha viambishi katika kitenzi kifuatacho : Alijikatia ( alama3)

d)Tunga sentensi tatu kuonyesha matumizi matatu ya kiambishi ' **li'** . (alama3)

e)Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kipungufu katika ngeli ya **KU**( alama 2)

f)Mtume ni tamko la kuonyesha mshutuko , ____________________ ni tamko la kuonyesha kuridhika ( alama 1)

g)Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo .

i) Wanafunzi wengine wameadhibiwa ( Tumia kiwakilishi) ( alama 1)

ii)Mtoto alimpiga mbwa kwa kijiti (Andika katika ukubwa wingi ) ( alama 2)

h)Tunga sentensi ukitumia kiunganishi cha kujumuisha. ( alama 2)

i)Tunga sentensi ukitumia neno "**mpaka**" kama,

i)Kihusishi cha kiwango ( alama 1)

ii)Kihusshi cha wakati ( alama 1)

j)Tambua na ueleze virai katika sentensi ifuatayo: ( alama 3)

Kischana kile kimejirembesha kwa manukato mazuri ajabu.

k)Tunga sentensi yenye muundo ufuatao ( alama 4)

i) RN + RT

ii)Nomino + Kivumishi + Kivumishi + Kishazi tegemezi + Kitenzi kishirikishi + Kivumishi

l). Tunga sentensi ukitumia kielezi mfanano ( alama 2)

m)) Yakinisha sentensi ifuatayo :

Nisipomwona darasani sitampa kitabu chake. ( alama 2)

n) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu . ( alama 2)

Dobi huwapigia watu nguo pasi .

o) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya ritifaa. ( alama 2)

p) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo:

Msichana aliitwa mara nyingi . (alama 1)

q). Tunga sentensi katika hali ya amri wingi ( alama 1 )

r) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa.

“Nitampokea mjomba iwapo nitampata.’’Rehema alimwambia shangazi yake. ( alama 2)

s) Eleza maana **mbili** ya neno ‘pora’ ( alama 1)

## MTIHANI WA PILI

(a) Andika neno lenye silabi mbili za irabu. (alama 1)

(b) Ni sauti gani haifai kuwa miongoni mwa hizi? Toa sababu. (alama 2)

/ng’/, /g/, /t/, /k/

(c) Tunga sentensi mbili tofauti kwa kutumia neno walakini kama: (alama 2)

(i) kiunganishi

(ii) nomino

(d) Panga maneno yafuatayo ili kutunga sentensi sahihi ya Kiswahili. (alama 2)

Walikataliwa wanasiasa baadhi ya katika nchi wachache uhasama waliochochea.

(e) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo

Hakumjia (alama 3)

(f) Tambua shamirisho katika sentensi hii

Chema alimuuzia mtalii wa Kimarekani leso za Kimaasai. (alama 2)

(g) Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia o – rejeshi tamati katika wingi. (alama 2)

Kambare amenaswa demani.

Kambare atauzwa sokoni.

(h) Tunga sentensi yenye kivumishi cha jina. (alama 2)

(i) Changanua kwa jedwali

Kama atasoma kwa bidii, atapita mtihani. (alama 3)

(j) Tunga sentensi sahihi ukitumia visawe vya neno 'dalali'. (alama 1)

(k) Andika udongo wingi wa sentensi ifuatayo

Njia hii inafaa zaidi kuliko ile. (alama 2)

(l) Mwajiri wao amekuja kuwalipa mshahara. (Andika katika hali ya ukatavu) (alama 2)

(m) Andika sentensi hii upya ukitumia chagizo cha wakati. (alama 1)

Bata alienda mjini.

(n) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. (alama 2)

Moraa alituahidi kuwa angetutembelea mwaka ambao ungefuata.

(o) Andika upya kulingana na maagizo (alama 2)

(i) Mgonjwa amelazwa hospitalini (kutendesheka)

(ii) Mama ameinjika chungu mekoni. (tendua)

(p) Andika miundo miwili ya kirai nomino. (alama 2)

(q) Mbali na kutumika mwanzoni mwa sentensi na nomino za pekee, eleza matumizi

mengine mawili ya herufi kubwa. (alama 2)

(r) Kwa kutoa mifano, onyesha miundo mitatu ya ngeli ya U – ZI. (alama 3)

(s) Onyesha matumizi mawili ya kiambishi {i} (alama 2)

(t) Tumia kishazi tegemezi katika sentensi kuvumisha nomino. (alama 2)

## MTIHANI WA TATU

(a) Silabi ni nini? (alama 2)

(b) Andika kinyume cha:

Msichana aliingia darasani kwa haraka. (alama 2)

(c) Tambua viambishi awali na tamati katika kitenzi:

Aliyemlia (alama 2)

(d) Akifisha:

sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote alifoka abdi (alama 3)

(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (alama 4)

Wote warefu ni wanafunzi.

(f) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii:

Nyumba iliyojengwa jana imebomolewa. (alama 2)

(g) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizoko kwenye mabano.

(i) –fa(fanyia) (alama 1)

(ii) soma (tendesheana) (alama 1)

(h) Ainisha vielezi katika sentensi ifuatayo:

Juma alitukumbusha alivyotutembelea mara kadha mwaka jana. (alama 2)

(i)Onyesha aina ya shamirisho katika sentensi:

Mzazi alimbebea mtoto vitabu kwa mkoba. (alama 3)

(j) Tambua aina ya vitenzi katika sentensi:

Amekuwa akilala kwa vile yu mgonjwa. (alama 3)

(k) Taja na utofautishe vipasuo vya ufizi. . (alama 2)

(l) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari.

**Amegura** mjini kwa sababu ya **mvulana** huyo. . (alama 3)

(m) Yakinisha:

Hajanivunjia mlango wala kuniibia. (alama 2)

(n) Onyesha aina za nomino katika sentensi ifuatayo na utambue zimo katika ngeli gani.

Kamati iliushuku werevu wake. (alama 2)

(o) Toa maana mbili za sentensi:

Alisimamisha gari njiani. (alama 2)

(p) Eleza matumizi ya "na" katika sentensi:

Njambi na Halima wanaandaliwa chakula na Hamedi. (alama 3)

(q) Tumia mzizi "enye" katika sentensi kama kiwakilishi. (alama 1)

## MTIHANI WA NNE

(a) (i) Eleza maana ya sauti mwambatano kisha utolee mifano. (alama 2)

(ii) Eleza sifa tatu za sauti /i/ (alama 3)

(b) (i) Tofautisha mofimu na kiambishi. (alama 2)

(ii) Bainisha mofimu katika neno: mjamwema. (alama 2)

(c) Ainisha maneno katika sentensi hii. (alama 2)

Je, umewahi kumwona yule?

(d) Kwa kutoa mfano mwafaka, eleza maana ya silabi funge. (alama 2)

(e) (i) Shamirisho ni nini? (alama 2)

(ii) Andika sentensi hii upya ukigeuza yambiwa kuwa kiima. (alama 2)

Mzazi alipigiwa simu na mwalimu kwa furaha.

(f) Yakinisha katika wingi sentensi hii. (alama 2)

Mama alikuwa hajaingia kanisani.

(g) (i) Eleza maana ya kishazi. (alama 2)

(ii) Tunga sentensi moja inayoundwa na vishazi tegemezi pekee. (alama 2)

(h) Tunga sentensi zitakazoeleza maana mbili za alama hii ya uakifishaji. (alama 2)

Herufi nzito

(i) Tunga sentensi yenye muundo huu wa maneno. (alama 2)

S – KN (W+ $\bar{S}$) + KT ( t+V)

(j) Eleza sifa mbili za nomino katika ngeli ya U – YA. (alama 2)

(k) Sahihisha sentensi hii. (alama 1)

Niliingia hotelini nikatumana mhudumu aniletee chakula.

(l) Tunga sentensi moja ili kubainisha maana mbili za neno:oza. (alama 2)

(m) Taja methali moja yenye maana sawa na nahau hii: (alama 1)

Kuchanga bia

(n) Kanusha:

Kwenda kwake kazini kulimfanya apandishwe cheo. (alama 1)

(o) Bainisha viambishi katika neno: angechomolewa.

(i) Kimuundo (alama 1)

(ii) Kidhamira (alama 2)

(p) Andika katika usemi halisi. (alama 3)

Mshtakiwa alidai kwamba alikuwa ameonewa kwa kuwa hakuwa ameshiriki ulevi kutoka mwaka uliokuwa umetangulia.

# MTIHANI WA TANO

(a)Toa maelezo ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti hizi. (al 2)

(b) Tenga silabi katika neno: Alimhukumu. (alama 1)

(c)Tunga sentensi moja yenye kitenzi shirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba. (al 3)

(d) Tumia neno mji kama kielezi cha mfanano. (alama 1)

(e) Onyesha namna tatu za kutumia kiambishi "ji" katika sentensi moja, kisha ueleze matumizi husika. (alama 3)

(f) Ziweke nomino hizi katika ngeli zake. (alama 2)

mtaji

Insi

(g) Tambua virai vilivyopigiwa mistari ni vya aina gani na uonyeshe miundo yake. (alama 4)

(i) Kikapu kilichofumwa juzi kitauzwa marikiti.

(ii) Wenzetu walikuwa wakijinaki kabla ya dimba.

(h) Eleza maana mbili za sentensi: Zainabu alisema atakusaidia. (alama 2)

(i) Onyesha majuku ya mofimu katika neno: awaliaye (alama 3)

(j) Andika kinyume: Aliiangika picha ukutani baada ya sherehe. (alama 2)

(k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo bila kutumia kiambishi ku. (alama 2)

(l) Eleza tofauti iliyopo kati ya ukanushaji na kinyume. (alama 2)

(m) "Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu", mpishi alalamika. (alama 2)

(n) Tumia visanduku kuchangana sentensi ifuatayo. (alama 4)

Alipotuona alitupuuza lakini sisi tulimsalimia.

(o) Tumia vitate vya jua, toa na baka katika sentensi mbili tofauti. (alama 3)

(p) Kamilisha kwa viigizi mwafaka. (alama 2)

(i) Ameanguka__________ matopeni.

(ii) Mlango ulipishwa ______________

(q) Tofautisha sentensi. (alama 2)

(i) Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.

(ii) Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.

# MTIHANI WA SITA

(a) Tumia neno Kamene kama yambiwa katika sentensi. (alama 2)

(b) Taja misingi ya upangaji wa irabi za Kiswahili. (alama 3)

(c) Huku ukitoa mfano mmoja, eleza maana ya mofimu ya kimsamiati. (alama 2)

(d) Vitambue vijenzi vya kimsingi vya lugha ya Kiswahili. (alama 2)

(e) (i) Eleza maana ya kishazi. (alama 1)

(ii) Tunga sentensi moja yenye kishazi tegemezi kinachovumisha. (alama 2)

(f) Badilisha kitenzi kisaidizi kilicho kwenye sentensi ifuatayo kiwe kishirikishi. (alama 2)

Mvule alikuwa akilala bwenini.

(g) Taja majukumu ya vipengele vilivyopigwa kijistari. (alama 4)

<u>N</u>anyi nende<u>ni</u> haraka au muadhibiwe <u>k</u>inyama <u>kwa</u> utundu wenu.

(h) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa. (alama 2)

Uteo alionunuliwa umezeeka sana.

(i) Tunga sentensi moja mwafaka kudhihirisha matumizi ya kiunganishi madhali. (alama 2)

(j) Onyesha minyambuliko ya maneno yafuatayo katika kauli zilizotolewa mabanoni. (alama 2)

(i) ja (tendewa) ………………………………………………………………………………………

(ii) cha (tendeka) ………………………………………………………………………………………

(k) Katika sentensi moja, onyesha matumizi mawili ya kibainishi. (alama 2)

(l) Yakinisha (alama 2)

Usipolipa usiingie ndani

(m) Neno ‘gofu’ linapatikana katika ngeli gani? (alama 1)

(n) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. (alama 2)

Kassim alimwomba Hirshi aende mahali alipokuwa ili amtume.

(o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo matawi. (alama 4)

Japo Mutiso anasinzia darasani hajamaliza kazi yake.

(p) Iandike upya sentensi ifuatayo kwa kutumia visawe vya maneno yaliyo katika italiki. (alama 3)

*Mdarisi* aliwashauri wanafunzi kuwa *bidii* huzaa *ufanisi*

(q) Unda kitenzi kutokana na kivumishi jasiri. (alama1)

(r) Andika maana ya nahau: kunjua jamvi (alama 1)

## MTIHANI WA SABA

(a) (i) Eleza jinsi kitamkwa /u/ kinavyozuliwa (alama 2)

(ii) Andika tofauti moja kati ya sauti hizi. (alama 1)

/t/ na /d/

(b) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mwanajamii yule alijibu maswali yote kwa makini.

(c) (i) Eleza maana ya vitenzi vishirikishi. (alama 1)

(ii) Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina mbili za vitenzi vishirikishi. (alama 2)

(d) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama 1)

Mtoto hakufundishwa wala kupewa vitabu.

(e) (i) Eleza maana ya silabi. (alama 1)

(ii) Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)

(f) Ainisha viambishi katika sentensi hii kimuundo na kidhamira. (alama 3)

Wataonana

(i) Kimuundo:

(ii) Kidhamira

Tumia nomino yoyote katika ngeli ya KU-KU pamoja na kiashiria kisisitizi cha karibu kutunga sentensi. (alama 1)

(g) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali isiyodhihirika (alama 1)

(h) Tunga sentensi mbili ili kubainisha maana za neno: Jinsi (alama 2)

(i) Huku ukitoa mifano, eleza matumizi mawili ya alama ya kinyota katika uakifishaji. (alama 2)

(j) Eleza miundo mitatu ya vishazi tegemezi na kuitolea mifano mwafaka katika sentensi. (alama 3)

(l) (i) Eleza maana ya shamirisho kipozi. (alama1)

(ii) Benta alimlimia mamake shamba kwa trekta. Anza kwa yambiwa (alama1)

(m) (i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.

S – KN (N/Wθ) + KT (Ts+T+RH+E) (alama 2)

(ii) Changanua kwa matawi sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kile chake kipya kinanipendeza mno.

(n) Eleza matumizi yoyote mawili ya kiambishi KU na kuyatolea mfano mmoja mmoja wa sentensi. (alama 2)

(o)Tunga sentensi sahihi ukitumia kivumishi cha ki ya mfanano na kielezi cha namna kitumizi. (alama 2)

(p)Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha silabi moja kinachomaanisha kuogopa katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

(q) Eleza maana ya:

(i) Papo kwa papo kamba hukata jiwe. (alama 1)

(ii) Ua langu la waridi limechanuka. (alama 1)

(r) (i) Tunasema baraza la wazee …………………cha kuni na ……………..…… ya nguo (alama 1)

(ii) Ajuza ni kwa mwanamke mzee na …………………ni kwa msichana mchanga ilhali shaibu ni kwa mwanamume mzee na ………………………ni kwa mvulana aliyebaleghe. (alama 1)

## MTIHANI WA NANE

a) Bainisha sifa zinazotofautisha sauti zifuatazo: (alama 2)
/e/ na /u/

b) Pigia mstari silabi inayowekwa shadda katika tungo lifuatalo: (alama 1)
Walituchochea

c) Tunga sentensi moja kubainisha kiwakilishi kiambata nafsi ya kwanza wingi. (alama 2)

d) Taja matumizi <u>manne</u> ya kiimbo. (alama 2)

e) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya kistari kifupi (-). (alama 2)

f) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 4)
'Mbona unamfanyia karaha mwenzako? Je, utaenda kumwomba radhi?' Phanice aliuliza.

g) Andika katika hali ya mazoea. (alama 2)
Mtambo ambao unakarabatiwa leo utatufaa.

h) Andika kwa ukubwa wingi. (alama 2)

Mke wa mzee huyu hupenda mtoto huyu sana.

i) Changanua kwa kutumia mtindo wa jedwali. (alama 4)

Wazazi wengi sana waliofika shuleni mapema walileta vyakula vingi sana.

j) Yakinisha sentensi hii katika umoja. (alama 2)

Msipohama hapa hamtapewa makazi mapya

k) Onyesha kiima, chagizo na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 3)

Mkulima alimfungia mwajiri ng'ombe kondeni.

l) Tunga sentensi ukitumia kitenzi 'pwa' katika kauli ya kutendea. (alama 2)

m) Eleza matumizi ya 'ji' katika sentnsi hii. (alama 2)

Mwimbaji amejikata jidole lake kwa jiwe.

n) Tunga sentensi moja ukitumia kinyume cha neno 'lewa'. (alama 2)

o) Tunga sentensi yenye kiigizi na kihusishi cha mahali. (alama 2)

## **MTIHANI WA TISA**

(a) Bainisha sauti mbili aina ya likwidi. (ala2)

(b) Andika upya sentensi ifuatayo ukitujmia -0- rejeshi tamati. (ala1)

Debe ambalo humwaga maji lina tundu.

(c) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi 'dhalimu' (ala2)

(d) Neno 'kiongozi' ni mofimu aina gani? (ala1)

(e) Ainisha yambwa katika sentensi : (ala2)
Shivambo alimnunulia babake simu.

(f) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentEnsi tatanishi. (ala2)

(g) Iweke nomino 'pua' katika ngeli yake. (ala1)

(h) Eleza matumizi ya 'li' kama ilivyotumika katika sentansi ifuatayo: (ala1)
Tunda li mezani

(i) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha jumla katika ngeli ya KI-VI. (ala2)

(j) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia matawi. (ala4)
Amina hakwenda shuleni wala kuhudhuria ibada.

(k) Tumia kwa kutunga sentensi kuonyesha: (ala2)

(i) Kitumizi

(ii) Umilikaji

(l) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (ala2)

Amefundishwa kupika vizuri na mamake.

m) Eleza tofauti kati ya sentensi hizi. (ala2)

Angeimba vizuri angetuzwa

Angeliimba vizuri angelituzwa

(n) Tumga sentensi kuonyesha tofauti kati ya.

Landa na Randa

(o) Kitenzi kwama kiko kauli (hali ) ya

(p) (i) Nini maana ya nomino dhahania. (ala1)

(ii) Toa mfano mmoja wa nomino dhahania. (ala1)

(q) Ukitoa mifano mwafaka, onyesha matumizi mawili ya koloni(☺ katika sarufi ya Kiswahili.

(r) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.

"Mzee, gari la moshi huondoka hapa saa ngapi?'' Mgeni aliuliza.

(s) Andika kinyume cha sentensi hii. (ala2)

Kijakazi alihuzunika mtoto alipopotea.

(t) Taja na ueleze aina ya kielezi kilichotumika katika sentensi. (ala2)

Wanafunzi waadilifu washauriwa watembee makundimakundi

# MTIHANI WA KUMI

1. Eleza sifa bainifu za sauti /j/. (al 2)
2. Tofautisha mofimu huru na tegemezi kwa kutolea mifano mwafaka. (al 2)
3. Unda neno lenye silabi ifuatayo KIKKIKI (al 1)
4. Tia shadda katika sentensi ifuatayo (al 1)

   *Wachezaji wamo uwanjani*.
5. (i) Kiimbo ni nini? (al 1)

   (ii) Onyesha matumizi mawili ya kiimbo. (al 2)

   Ainisha (al 3)

   Wasiorithishwa
6. Sahihisha sentensi ifuatayo. (al 2)

   *Sukari zilizowekwa mfukoni zimenyeshewa*
7. Eleza maana ya sentensi zifuatazo. (al 2)

   (i) Tunda lenyewe limeoza

   (ii) Tunda lenye shimo halinunuliki
8. Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

   Ningalifuzu katika mtihani wangu ningalituzwa.
9. Tunga sentensi na ubainishe kijalizo. (al 2)
10. Andika sentensi usemi halisi.

    Rais alisema kuwa wangepata tiba ya bure kama bunge lingepitisha mswada huo.
11. Tunga sentensi yenye muundo wa: (al 3)

    Kiima, kiarifa, yambwa tendwa, yambwa tendewa na yambua ala.
12. Changanua sentensi kwa kutumia jedwali. (al 4)

    Wachezaji vikapu watakifanikiwa katika mechi hiyo watatuzwa medali
13. Nyambua kitenzi hiki katika kauli iliyo mabanoni *pa* (tendeka) (al 1)
14. Bainisha virai katika sentensi hii. (al 3)

    Juma alikwenda mjini kwa miguu
15. Tunga sentensi kudhihirisha matumizi mawili ya KU. (al 2)
16. Onyesha matumizi mawili ya nukta mkato. (al 2)
17. Toa maana mbili ya sentensi ifuatayo: (al 2)

    Laleni!

p) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti ya maana kati ya 'guna' na 'kuna' (alama 2)

q) Ainisha vitenzi katika tungo lifuatalo. (alama 2)

Huyu alikuwa angali bwenini.

r) Unganisha sentensi hizi ukitumia kiunganishi cha kinyume. (alama 2)

Wananchi walikabiliwa na hatari

Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.

## MTIHANI WA KUMI NA MOJA

1. Tambua vigezo vya kuainisha irabu. (alama 2)
2. Eleza maana ya kundi nomino. (alama 2)
3. Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

   Mtoto alipikiwa uji na mamake jana jioni kwa jiko.
4. Andika maana mbili za neno mradi. (alama 2)
5. Kuza sentensi ifuatayo. (alama 2)

   Nguo iliyoraruka itashonwa tena na fundi
6. Andika kulingana na maagizo (alama 2)

   (Tumia wakati usiodhihirika)

   Mwanafunzi anazungumza kiingereza vizuri.
7. Tofautisha sentensi zifuatazo kwa kutia shadda (alama 2)

   Wataka kazi

   Wataka kazi
8. Tunga sentensi ukitumia neno ganda katika kauli ya kutendana. (alama 1)
9. Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo. (alama 2)

   Askari alimkimbilia mwizi.
10. Yakinisha katika nafsi ya pili umoja (alama 2)

    Tusipoonana na mgeni hatutafaidi
11. Unda kitenzi kutokana na neno bora na utunge sentensi katika hali ya wingi. (alama 2)
12. Tofautisha (alama 2)

    Mkulima amekula tunda lolote

    Mkulima amekula tunda lote
13. Changanua kwa jedwali (alama 2)

Chakula ambacho kilipikwa vizuri kimeliwa na watu wote

14. Tambua matumizi ya ni – katika sentensi hii (alama 2)

Mwanafunzi ni mtukutu

Ameenda ibadani

15. Kanusha (alama 2)

Nikimwona ndugu yangu nitamjulisha habari hizi

16. Tambua aina ya nomino katika utungo ufuatao. (alama 3)

Mji wa sokomoko una masaibu mengi

17. Linganisha na ulinganue sauti /k/na/g/ (alama 2)

18. Tambua mofimu katika neno lifuatalo (alama 2)

Waimbao

19. Tambua aina mbili ya virai katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Mwanafunzi shupavu aliponea chupuchupu

20. Andika sentensi ifuatayo upya kwa mwanzo wa kiwakilishi (alama 1)

Mama huyu anapika wali

Tumia ‘O’ rejeshi tamati (alama 1)

Nguo iliyonunuliwa si ile uliyoitaka

## MTIHANI WA KUMI NA MBILI

a) Tofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)

/a/

/u/

b) i) Ngeli ni nini? (alama 1)

ii) Maneno haya yamo katika ngeli gani? (alama 2)

Tayo

Kipepeo

c) Akifisha sentensi hii kwa njia tatu tofauti kuleta dhana tatu tofauti. (alama 3)

Babu alimchapa nyanya

d) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo (alama 3)

Sikumkaribisha

e) Andika katika usemi wa taarifa (alama 3)

"Mtapata mwaliko wenu kesho," alisema Salim

f) Andika kwa wastani (alama 2)

Magoma hayo yatachezwa mawanjani

g) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari

Wanafunzi wenye bidii hufuzu mtihani

h) Tofautisha sentensi zifuatazo. (alama 2)

i) Ningekuwa na pesa ningenunua simu nzuri

ii) Ningalikuwa na pesa ningalinunua simu nzuri

i) Tunga sentensi ukitumia vihusishi vya: (alama 3)

a) Kulinganisha

b) Sababu

c) Wakati

j) Kwa kutoa mifano katika sentensi onyesha matumizi mawili ya parandesi (alama 2)

k) Tambua kiima, shamirisho, chagizo na kiarifa katika sentensi ifuatayo (alama 4)

Nyanya alimjengea mjukuu nyumba kwa matofali mwaka jana.

l) Eleza tofauti ya kimaana katika sentensi hizi (alama 2)

i) Nisimamapo huchekwa

ii) Ninaposimama huchekwa

m) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia 'o' rejeshi na kiambishi ngeli

mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

n) i) Eleza dhana ya kishazi tegemezi (alama1)

ii) Bainisha aina za vishazi (alama 2)

Konde iliyopaliliwa ilituletea mazao mengi sana

o) Tunga sentensi kuonyesha maana mbili za neno chuma (alama 2)

# MTIHANI WA KUMI NA TATU

1. Andika sifa bainifu za /**d**/ na /**f**/. (alama 2)
2. **Andika kinyume cha sentensi hii**. (alama 2)

   Mama alianika nguo zilizofuliwa na Kitwana.
3. **Andika neno 'kuja' katika hali ya kuamuru.** (alama 1)
4. **Weka shadda katika neno 'nta'.** (alama 1)
5. **Yakinisha sentensi ifuatayo.** (alama 2)

   Wanafunzi wasipopita mtihani huo mwalimu hatalaumiwa.
6. **Kwa kutolea mifano, eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili.** (alama 3)
7. **Andika kwa udogo.** (alama 2)

   Chaka la Samba halilali paka.
8. **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.** (alama 4)

   Kiongozi aliyeng'olewa mamlakani amekufa.
9. **Mzizi ni nini? Toa mfano.** (alama 2)
10. **Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari.** (alama 2)

    Mjadala <u>huo mzuri</u> uliisha <u>usiku wa manane</u>.
11. **Tofautisha sentensi hizi:** (alama 2)
    a) Ningeondoka sasa ningefika mapema.
    b) Ningaliondoka sasa ningalifika mapema.
12. **Toa maana mbili za sentensi hii.** (alama 2)

    Aliletewa ng'ombe na mtoto wake.
13. **Tunga sentensi moja kubainisha.** (alama 2)

    Kivumishi cha pekee cha kusisitiza.
14. **Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano**. (alama 2)
    a) la (fanyia)
    b) suka (tendata)
15. **Fafanua aina ya hali zilizotumika katika sentensi hizi.** (alama 3)
    a) Mumo akacheka, akafurahia na akalala.
    b) Mtoto wa Maria hulia kila mara.
    c) Mwalimu aandika ubaoni.
16. **Tumia neno 'karibu' katika sentensi kama**: (alama 2)

a) Kihusishi

b) Kihisishi

17. **Tenganisha mofimu katika neno lifuatalo kisha uonyeshe majukumu yake kisarufi.** (alama 3)

    Onana

18. **Bainisha yambwa katika sentensi hii.** (alama 2)

    Simu aliyonunuliwa Ali na mjombake imepotea.

19. **Tumia kivumishi kionyeshi cha mbali pamoja na nomino katika ngeli ya I–I.**(alama 1)

# MTIHANI WA KUMI NA NNE

a) Taja sifa tatu kuu za sauti /k/ (alama 3)

b) Andika sentensi hii katika msemo halisi

   Mwalimu alimuambia mwanafunzi amalize kazi hiyo haraka (alama 2)

c) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya silabi funge (alama 2)

d) Weka nomino hizi katika ngeli zake (alama 2)

   Mbalungi

   Mturuki

e) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi, wakati uliopita hali ya kuendelea (alama 2)

   Mwalimu humuadhibu mwanafunzi mwenye hatia.

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali (alama 4)

   Omondi anaazimia kuwa mhasibu Lakini hatii bidii masomoni

g) Yakinisha katika nafsi ya tatu wingi (alama 2)

   Sijasafiri kwenda marekani

h) Bainisha matumizi ya kiambishi ‘ku’ katika sentensi hii (alama 2)

   Naomi atakupikia chai alafu aende kule uwanjani

i) Onyesha virai katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani. (alama 2)

   i) Anachukia kusoma riwaya yenye masuala ya kisiasa.

   ii) Watoto wa kike hudunishwa katika jamii nyingi

j) Onyesha matumizi mawili ya alama zifuatazo za uakifishaji (alama 4)

   Koloni (:)

   Kistari kifupi (-)

k) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo.

Walimu ni watu wasiopendwa wanaposema ukweli kuhusu wanafunzi (alama 3)

l) Eleza sifa mbili za vishazi tegemezi (alama 2)

m) Onyesha matumizi ya kiimbo katika sentensi hii

Ondoka hapa! (alama1)

n) Andika neno lenye maana sawa na (alama 2)

Hawala

Katani

o) Eleza maana ya sentensi hii (alama 2)

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari na ningalistarehe.

p) Eleza tofauti iliyopo kati ya sentensi hizi (alama 2)

Tulipofika hotelini tulipewa soda na chupa

Tulipofika hotelini tulipewa soda kwa chupa

q) Kanusha katika ukubwa ( alama 1)

Mwizi huyu aliiba kisu na ng'ombe wa mwanamke yule.

## <u>MTIHANI WA KUMI NA TANO</u>

a) Eleza sifa mbili za sauti /b/ (Alama 2)

b) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (Alama 2)

Nomino ya kawaida + Kivumishi + Kitenzi + Nomino ya wingi

c) Tunga sentensi ukitumia vihusishi vifuatavyo: (Alama 2)

i) Mtawalia

ii) Mkabala

d) Bainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo: (Alama 3)

Mwanafunzi aliyetaka kusoma yu darasani.

e) i) Kirai ni nini? (Alama 1)

ii) Tunga sentensi moja moja kwa kutumia: (Alama 2)

Kirai kihusishi

Kirai kivumishi

f) Eleza dhana inayojitokeza katika sentensi hii: (Alama 2)

Tokeni! Na mwende kabisa.

g) Eleza matumizi ya kiambishi **ku** katika sentensi uliyopewa: (Alama 3)

Baba mzazi ana**ku**ita uende **ku**pika **ku**liko watu wengi.

h) Bainisha kiima na kiarifa katika sentensi hii: (Alama 2)

Mhubiri huyu atahubiri kesho jioni.

i) Onyesha shamirisho kipozi, shamirisho kitondo na shamirisho ala katika sentensi ifuatayo:

Mkurugenzi aliwalipia wafanyikazi nauli ya kwenda Mombasa kwa ndege. (Alama 3)

j) Andika visawe vya maneno haya: (Alama 2)

i) Duara

ii) Fedha

k) Dhihirisha matumizi mawili ya alama ya kuakifisha ifuatayo (/) (Alama 2)

l) Kanusha sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa: (Alama 2)

Mbwa na ngamia ni wa manufaa sana.

m) Pambanua sentensi ifuatayo kwa kutumia visanduku: (Alama 4)

Mama aliyekifungoni amejifungua mtoto mzuri.

n) Tunga sentensi moja ukitumia neno mwalimu kama: (Alama 2)

i) Nomino

ii) Kivumishi

o) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendewa: (Alama 2)

i) Nywa

ii) Pa

p) Andika katika kauli ya taarifa sentensi uliyopewa: (Alama 2)

"Kuna umuhimu wa kuwaheshimu wakubwa wenu," Mwalimu aliwasisitizia wanafunzi.

q) Eleza dhana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii: (Alama 2)

Baba alisema kwamba ataenda kumwona

# MTIHANI WA KUMI NA SITA

a) Taja sifa za irabu hizi /i/ na /e/ (alama 2)

b) Tenganisha viambishi vilivyojenga neno lifuatalo: (alama 2)

Tunakumbuka

c) Vitenzi vya Kiswahili hugawika katika vikundi viwili vikuu. Vitaje. (alama 1)

d) Andika nomino mbili zinazoweza kuundwa kutokana na kitenzi ulichopewa: (alama 2)

Saili

e) Tambulisha matumizi ya ‘kwa’ katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Alisababisha ajali <u>kwa</u> ulevi wake.

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielelezo cha jedwali: (alama 4)

Omari atafika kesho jioni

g) Akifisha sentensi ifuatayo:

hoteli ya shelter afrique iliyoko jijini inapigwa mnada baada ya miezi miwili ya kufanya biashara (alama 2)

Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kuyakinisha:

Mchoraji hachori picha nzuri (alama 1)

Onyesha aina za nomino hizi: (alama 2)

Jini

Wizi

h) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo: (alama 1)

Meza

Linganisha

i) Andika sentensi ifuatayo upya kwa msemo wa taarifa: (alama 5)

“Sikiliza bwana mdogo, siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika. Hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote,” alifyoa Kameme.

j) Bainisha shamirisho kipozi na shamirisho kitondo katika sentensi hii: (alama 2)

Okoth alinunuliwa redio nzuri na mjomba wake aliyekuwa ng’ambo.

k) Kanusha neno hili: (alama 1)

Wakimenyanamenyana

l) Onyesha matumizi ya 'ni' katika sentensi hizi:

i) Yule mwanafunzi ni stadi sana (alama 2)

ii) Nitawapelekeni mahakamani

m) ifuatayo upya kwa kugeuza neno lililopigiwa mstari kuwa nomino: (alama 2)

Tulipokwenda hotelini tulikula chapati na nyama.

n) Bainisha mofimu katika neno lifuatalo: (alama 2)

Jimbi

o) Eleza matumizi ya 'ku' katika sentensi ifuatayo:

Kulikoharibika ni kwa kuogopwa (alama 2)

p) Sentensi ifuatayo inatekeleza jukumu lipi?

Acheni kucheka ovyo! (alama 2)

q) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi:

Yule mtoto asipoanguka, sitalaumiwa (alama 2)

r) Kiimbo ni nini? (alama 1)

## MTIHANI WA KUMI NA SABA

(a) Silabi ni nini? (al 2)

(b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

(i) igwa

(ii)Oa

(c) Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. (al 2)

(i) Galagala …………………………………………………………………………………

(ii) Teketeza ………………………………………………………………………………...

(d) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (al 2)

(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa

(ii)Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

(e) Eleza matumizi ya kihusishi kwa katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.

(f) Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. (al 2)

Siji.

(g) Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. (al 1)

Tepetevu

(h) Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme

(i) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Mzalendo amemwandikia mhariri barua.

(j) Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. (al 2)

Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani

(k) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

(l) Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo

(m) Andika katika wingi. (al 2)

Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.

(n) Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. (al 1)

Mhalifu huyu <u>alitunga</u> mimba

(o) Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. (al 1)

Jua limekuwa likiwaka tangu Januari

(p) Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: (al 1)

Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga

(q) Akifisha sentensi hii: (al 2)

Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo

(r) Badilisha katika usemi wa taarifa: (al 2)

“Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi,” afisa wa usalama akasem.

(s) Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. (al 1)

Aliyerembesha <u>uso</u> kwa poda.

(t) Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: (al 3)

Mwalimu amempigia wanafunzi simu

(u) Silabi mwambatano ni nini? (al 1)

(v) Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: <u>Rudi</u> (al 1)

(w) Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.

## MTIHANI WA KUMI NA NANE

(a) i.Taja vigezo viwili vya kuanisha irabu. (alama 1)

ii.Tofautisha sauti zifuatazo.(alama.2)

a. /a/ na /i/

b. /e/ na /o/

(b) Ainisha aina za vivumishi katika sentensi ifuatayo.(alama. 2)

Mwalimu mzee alitufundisha vizuri ile mada ngumu.

i. i.Eleza maana ya kirai. (alama.1)

ii. Tunga sentensi iliyo na kirai kivumishi na kirai nomino chenye muundo wa W+ V (alama 1)

(c) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia “O” rejeshi. (alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

(d) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya udogo wingi.

Kono lake lilivimba baada ya kuumwa na jibwa. (alama 2)

(e) Tunga sentensi iliyo:(alama 3)

Kitenzi kishirikishi kikamilifu

Kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi

Kiwakilishi cha nafsi ya tatu tegemezi wingi.

(f) Kanusha sentensi ifuatayo kisha ueleze maana yake katika hali kanushi (alama 2)

Angeongoza darasa lake, angepewa tuzo.

(g) Onyesha sehemu za kisarufi katika neno lifuatalo. (alama 2)

Kililiwa

(h) Kanusha katika hali timilifu wakati uliopita.

Kamati ya uchaguzi iliandaa ripoti kuhusu utovu wa nidhamu shuleni.(alama 2)

(i) Changanua kwa kutumia mchoro wa matawi

Hatukuondoka na yeye japo tulirudi naye. (alama 4)

(j) Tumia kiambishi KA katika sentensi ili kuleta dhana ya: (alama 2)

i. Wakati usiodhihirika

ii. Kuonyesha matokeo yanayosababishwa na kitendo.

(k) Chane kwa mtama_________________ kwa udongo. (alama 1)

(l) a. Eleza maana ya fungu tenzi. (alama 1)

b.Taja aina mbili za fungu tenzi.(alama.2)

(m)Geuza sentensi hii hadi usemi halisi.

Wanakijiji walikuwa wanataka kujua iwapo vipakatalishi vya shule za msingi vingeweza kuinua kiwango cha elimu. (alama 3)

(n) a. Eleza maana ya yambwa.(alama 1)

b. Tunga sentensi iliyo na: shamirisho kipozi na chagizo cha kiasi kamili. (alama.2)

(o) Tunga sentensi kwa kutumia kiunganishi cha wakati.(alama 2)

(p) Andika visawe vya maneno yaliyopigigwa mstari. (alama 2)

Tulienda <u>kusali</u> siku ya <u>Jumapili.</u>

## MTIHANI WA KUMI NA TISA

a) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. [alama 3]

Raisi alisema kuwa angesafiri kwenda Somalia siku hiyo alasiri.

b) Andika neno lenye muundo ufuatao. [alama 2]

Kiambishi ngel,i wakati ujao, mzizi, kauli tendwa, kauli tenda (kiishio )

c) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. [alama 3]

Juma alipakuliwa chakula kwa bakuli.

d) Tumia neno mume kama kielizi katika sentensi. [alama 2]

e) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi. [alama 2]

f) Tunga sentensi yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu. [alama 1]

g) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu/dhamira yake. [alama 1]

Funga majani matatu matatu kwa kila fungu.

h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. [alama 2]

i) la - (tendeana)

ii) Vaa (tendwa)

I) Onyesha matumizi ya kiambishi ‘ku’ katika sentensi ifuatayo. [alama 2]

Juma atakutengenezea mpini wa jembe kisha aelekee kule kwao.

j) Onyesha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo. [alama 2]

Wanafunzi wale walijibu maswali kwa utaratibu.

k) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi, wakati uliopita hali ya kuendelea. [alama 2]

Mwalimu humwadhibu mwanafunzi mwenye hatia.

l) Tenga viambishi na mzizi katika neno ‘Siji’. [alama 2]

m) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali. [alama 4]

Nilimwona mamba majini nilipopiga mbizi.

n) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari katika kinyume. [alama 2]

Mwanafunzi aliketi kisha akakitega kitendawili.

o) Eleza tofauti kati ya sentensi hizi. [alama 2]

“ Ningefika mapema ningemkuta mwalimu darasani.

Ningalifika mapema ningalimkuta mwalimu darasani.

p) Andika visawe vya maneno haya. [alama 2]

i) Heshima

ii) Ruhusa

q) Bainisha mofimu katika neno wafiwa. [alama 2]

v) Andika sauti zenye sifa zifuatazo. [alama 2]

i) Kikwamizo ghuna cha mdomo na meno.

ii) Irabu ya nyuma, wastani.

s) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo-;

Jua lile ni muhimu kwetu.

# MTIHANI WA ISHIRINI

**3. MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: (alama2)
   i) nazali ya kaakaa gumu…………………………………………………………...
   ii) kikwamizo ghuna cha kaakaa laini……………………………………...
   iii) irabu ya mbele, wastani……………………………………………………..
   iv) kiyeyusho cha midomo…………………………………………………

b) Bainisha silabi katika neno: wachangamshwavyo. (alama 1)

c) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kubadilisha nomino zilizopigiwa mstari kuwa vitenzi.
Wachezaji wote watafanyiwa <u>ukaguzi</u> ili kupata <u>suluhu</u> ya matatizo hayo (alama 2)

d) Andika sentensi ifuatavyo katika umoja.
Tukishiriki katika maigizo hayo vizuri tutaweza kujishindia tuzo.
(alama 2)

e) Andika neno **moja** lenye viambajengo vifuatavyo: (alama 2)
nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita,yambwa, mzizi, kauli tendesha,kauli tenda

f) Tunga sentensi kuonyesha matumizi yafuatayo ya neno: ni (alama 2)
   i) kitenzi
   ii) kiwakilishi

g) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kivumishi. (alama 2)

h) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.
Nyundo hizo zimetupwa mbali na jumba lile. (alama 1)

i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama2)
Nomino ya wingi , kivumishi, kitenzi kishirikishi, kivumishi

j) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo.
Matunda yanayozalishwa kwa njia za kiasili yana virutubishi vingi. (alama 1)
Anza kwa: Virutubishi vingi

k) Tumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigiwa mstari.
<u>Mzee</u> atatembelea <u>mji</u> (alama 1)

l) Akifikisha sentensi ifuatayo:
basi mwanangu akasema cheusi hivyo ndivyo tunavyoweza kufikia gender parity wewe waonaje (alama 3)

m) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha wakati.
Idi alijishindia tuzo. Idi alishiriki katika uhifadhi wa mazingira. (alama 1)

n) Tumia 'kwa' katika sentensi kuonyesha: (alama 2)
   i) nia
   ii) pamoja na

o) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi.

Upepo ulivuma tulipokuwa tukiondoka. (alama 3)

p) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa.

Rono alicheza gitaa akiwa kwa Kiprono. (alama 2)

q) Onyesha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo:

Mumbi alitia embe kapuni likaiva. (alama 1)

...................................................................................................................................................

r) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea.
Mmomonyoko wa udongo ulipozuiliwa mashamba yalinawiri. (alama 2)

s) Tunga sentensi **moja** kutofautisha maana ya **baba na papa** (alama 2)

t) Methali: Haraka haraka haina baraka huambiwa mtu aliye na kasi isiyofaa katika kutenda mambo.Mtu anayepuuza shida za wenzake huambiwa aje? (alama 1)

u) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo: (alama 1)
Wale wageni walikipenda sana.

v) Andika kihisishi cha kuitikia wito kwa mtu wa jinsia ya kike (al 1)

w) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba tendo lilifanikiwa kwa sababu ya kufanikiwa kwa tendo lingine. (alama 1)

x) Andika miundo **miwili** ya nomino katika ngeli ya KI-VI. (alama 1)

y) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari. (alama 1)
Zana hizi zimeundwa <u>na mafundi</u> <u>wenye ustadi mkubwa</u>.

## MTIHANI WA ISHIRINI NA MOJA

a. i. Taja vigezo viwili vya kuainisha konsonanti. (Alama 1)
ii. Taja sifa mbili za sauti /o/. (Alama 2)

b. Andika sentensi ifuatayo ilete dhana mbili tofauti. (Alama 1)
Mwaura amekuja

c. Ainisha mofimu za sentensi ifuatayo. (Alama 3)
Amejilisha

d. Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza miundo mine ya nomino katika ngeli ya A-WA. (Alama 2)

e. Tambua viuakifishi vyenye matumizi yafuatayo:- (Alama 2)
   i. Hutumiwa kutenga msemaji na maneno au kauli yake.
   ii. Huonyesha kuwa sentensi ina makosa ya kisarufi.

f. Tambua aina ya maneno yaliyopigwa mstari.
   i. Mzee <u>mswahili</u> huvaa <u>Kiswahili</u>. (Alama 1)
   ii. Tunga sentensi kubainisha muundo ufuatao. (Alama 2)
   I+W+V+E+Ts+T+E

g. Andika kwa msemo wa taarifa. (Alama 2)

"Lo! Umeweza kuubeba mzigo huu pekeyo?" Mama alishangaa.

h. Andika sentensi ifuatayo katika udogo. (Alama 2)

Mtu yule haachi kuandamana na mbwa wake aliyedhoofika kiafya.

i. Tunga sentensi ukitumia visawe vya maneno haya. (Alama 2)

   i. Huzuni
   ii. Barua

j. Unda nomino dhahania kutoka vitenzi vifuatavyo. (Alama 2)

Pika

Lea

k. Tunga sentensi ukitumia kielezi cha nomino. (Alama 1)

l. Yakinisha sentensi zifuatazo. (Alama 2)

   i. Asipokuja hututaonana
   ii. Nisingalikuwa na uwezo nisingalinunua ndege.

m. Eleza matumizi ya 'po' katika sentensi hii. (Alama 2)

Mjomba aliniuliza "Je, sikukuambia kuwa akomelea<u>po m</u>wenyeji nawe mgeni koma pa<u>po.</u>

n. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (Alama 1)

Fundi aliezua paa la nyumba yetu.

o. Changanua sentensi hii kwa njia ya visanduku. (Alama 4)

Yule aliyechaguliwa alicheza mpira vizuri.

p. Tunga sentensi moja yenye shamirisho kitondo, shamirisho kipozi na shamirisho ala. (Alama 3)

q. Andika sentensi ifuatayo kwa umoja. (Alama 2)

Maovu waliotutendea hayatasahulika.

r. Andika sentensi upya kulingana na maagizo. (Alama 3)

   i. Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ikiwa unatumia msumeno. Anza: Ni rahisi…
   ii. "Kuna chai?" Mtoto aliuliza. (Maliza na … chai)

s. Fafanua chagizo katika sentensi hii. (Alama 1)

Kila mara Watende hakosi kuchezea Timu ya Taifa.

# MTIHANI WA ISHIRINI NA MBILI

a) Taja sauti moja ambayo ni kipasuo- kwaruzo hafifu cha kaakaa gumu (al.1)

b) Tofautisha kati ya silabi wazi na funge,huku ukitoa mfano mmoja mmoja (al.2)

c) Eleza matumizi mawili ya kiambishi "li" (al.2

d) Tunga sentensi mbili katika wingi ukitumia viunganishi vifuatavyo:(al.4)

   i. yamkini
   ii. labda

e) Huku ukitoa mifano mwafaka, onyesha maumbo matatu ya ngeli U-ZI. (al.3)

f) Onyesha vielezi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani. (al.2)

   i. Rajani alianguka mchangani pu!
   ii. Maria anapenda kurandaranda ovyo.

g) Hii sentensi ni aina gani? Thibitisha. (al.2)
Atakuwa akiimba na kurukaruka leo jioni,wageni waketipo mezani.

h) Ainisha mofimu katika neno hili .(al.4)
Aliyemcheleweshа

i) Tunga sentensi mbili kwa kutumia aina mbili za virejeshi. (al.4)

j) Iandike sentensi hii upya kwa kuanza na:kando ya barabara …
Mti mrefu umeanguka kando ya barabara . (al.2)

k) Changanua sentensi hii ukitumia jedwali Ijapokuwa yeye ni mweusi tititi, ni mrembo mno.

l) Tunga sentensi katika umoja ukitumia kuhusishi cha hali. (al.2)

m) Andika sentensi hii kwa msemo wa taarifa:
"Enyi wanafunzi watundu ,rudini nyumbani mwenu,mje kesho asubuhi na wazazi wenu," Mwalimu mkuu alisema kwa sauti ya juu. (al.3)

n) Nyambua vitenzi vifuatavyo kulingana maagizo katika mabano na kisha utungie sentensi katika hali uliyonyambua .(al.4)
a.Zoea (kutendeka)

b. Pata (kutendana)

o) Onyesha aina za shamirisho katika sentensi hii .(al.3)
Maria amelimiwa shamba lote na trekta ya oira.

p) Andika nomino moja kutokana na kitenzi hiki (al.1)

Tatua

# MTIHANI WA ISHIRINI NA TATU

**(a)Taja sauti zenye sifa zifuatazo. (alama 2)**

(i) King'ong'o cha mdomo:-------------------------------------------------------------------------------------------------

(ii) Irabu ya mbele kati:-------------------------------------------------------------------------------------------------

(iii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini:---------------------------------------------------------------------------------------

(iv) Kikwamizo sighuna cha menoni:-------------------------------------------------------------------------------------

**(b) Dhihirisha miundo ya silabi katika maneno yafuatayo. (alama 2)**

(i) itwa:------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

(ii) Mchwa:----------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**© Tunga sentensi mbili ili kuonyesha matumizi ya kiakifishi (alama 2)**

Vifungo

**(d) Andika sentensi ukitumia: (alama 2)**

(i)Kihusishi cha ulinganisho

(ii)Kihisishi cha furaha

**(e) Tunga sentensi ya neno moja iliyo na muundo ufuatao.(alama 2)**

(i)Nafsi

(ii)Mzizi

(iii)kauli

(iv)Kirejeshi

**(f)Eleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo. (alama 2)**

(i)Chakula <u>chochote</u> kitaliwa na watoto.

(ii) Chakula <u>chote</u> kitaliwa na watoto.

**(g) Kwa kutunga sentensi mwafaka onyesha aina tatu za yambwa. (alama 3)**

**(h)Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa.(alama 3)**

"Tutamtia mbaroni mhalifu huyo sasa hivi" Askari akasema.

**(i)Ainisha matumizi ya kiambishi "ji" katika sentensi (alama 3)**

Jibwa hilo liliweza kujinusuru kutokana na hasira za mkimbiaji.

**(j) Changanua kwa Jedwali. (alama 4)**

Otii ambaye hucheza mpira ni kijana mkali.

(k)Tofautisha vitate vifuatavyo kwa kuvitungia sentensi moja. (alama 2)

(i)Hawara:-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

(ii) Hawala:-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

(L) Bumba ni kwa nyuki---------------------------------------------------------------ni kwa samaki na---------------ni kwa siafu. (alama 2

**(m) Andika methali inayojumuisha ujumbe ufuatao.(alama 1)**

Hata mtaalamu huhitaji kutafuta msaada wa wataalamu wenzake.

**(n) Unda kitenzi kutokana na nomino zifuatazo. (alama 2)**

(i)Aina:------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

(ii)Moto-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**(O)Onyesha matumizi ya '<u>kwa</u>' katika sentensi. (alama 2)**

(i)Kwao kunawaka moto.

(ii) Magaidi walitoroka kwa kasi.

**(P) Nyambua katika kauli kwenye mabano. (alama 2)**

(i)Tua (tendama)

(ii) Pwa (tendeka)

**(q) Badilisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu. (alama 2)**

Mama huwapikia watoto chakula.

**(r) Tumia neno 'kesho' kutungia sentensi kama: (alama 2)**

(i)Nomino:------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

(ii) kielezi:-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------

# MTIHANI WA ISHIRINI NA NNE

(a)Linganisha na ulinganue sauti zifuatazo; (alama 3)

/b/ na /d/

(b)Tunga sentensi ukitumia vielezi vinavyotokana na maneno yafuatayo; (alama 2)

(i) Soko

(ii) Zidisha

(c ) Tunga sentensi ukitumia neno 'kuja' kama: (alama 2)

(i) Nomino
(ii) Kitenzi

(d) Tumia viambishi vitatu tofauti vya ngeli ya PA-KU-MU katika sentensi. (alama3 )

(e) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama3)

Watoto wanalipiwa karo na wazazi wao kwa hundi. (f)Neno "tikiti" hupatikana katika ngeli mbili. Zitaje. (alama 1)

(g)Andika kwa wakati ujao. (alama 2)

Ungalifanya kazi kwa bidii usingaliishi maisha ya dhiki.

(h) Onyesha matumizi tofauti ya 'PO' (alama 2)

(i)Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia vivumishi kulingana na maagizo kwenye mabano. (alama 3)

(i) Rehema ni bibi…………………………… bezo. (umilikaji)

(ii)Naomba kinywaji…………………………(ziada)

(ii)Muonye bawabu……………………………kwa kutofika mapema. (kusisitiza-mbali kidogo)

(j)Tunga sentensi ukitumia vitenzi ulivyopewa katika kauli ya kutendewa. (alama 2)

(i)Pa
(ii)nywa

(k)Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mistari au vishale. (alama 4)

Kibyego na Simiyu hucheza kandanda.

(l)Eleza maana mbili za sentensi hii. (alama 2)

Nenda ukaniletee daftari.

(m)Tunga sentensi ukitumia kielezi cha: (alama 2)

(i)Jumla

(ii)Namna linganisho

(n)Toa mfano wa neno lenye muundo wa silabi ya irabu pekee. (alama 1)

(o)Tunga sentensi ukitumia nomino ya wingi. (alama 2)

(p)Dhihirisha maana mbili tofauti za neno 'chupa' kwa kulitungia sentensi moja. (alama 2)

(q)Ainisha viambishi katika neno lifuatalo. (alama 2)

Aliyemwadhibu.

(r ) Akifisha. (alama 2)

Ndio tutahakikisha nyake amepata haki yake akamjibu.

## MTIHANI WA ISHIRINI NA TANO

a) Tofautisha irabu katika neno: **Pindu** (alama 2)

b) Eleza uamilifu wa viambishi katika neno: **wafiwao.** (alama 2)

c) Ziweke nomino zifuatazo katika ngeli zake: (alama 2)

i. Baridi ……………………………………………………………………………

ii) Undu …………………………………………………………………………

d) Eleza matumizi ya kwa katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Wazee kwa vijana walivuka barabara kwa makini ila sita kwa kumi ndio waliofika kwa Yohana

e) Tunga sentensi moja kubainisha matumizi mawili ya kiambishi **{ji}.(**alama 2)

f) Andika katika usemi wa taarifa: (alama 3)

“Kiwango cha umaskini katika gatuzi hili kinasikitisha sana; itabidi sote wakazi wa hapa tujizatiti ili tutimize malengo ya Milenia,”Seneta mteule alituhimiza.

g) Eleza maana tatu katika sentensi: Baba alimwanbia mtoto kuwa angeenda shuleni. (alama 3)

h) Ukizingatia kauli zilizo mabanoni tunga sentensi ukitumia vitenzi hivi. (alama 2)

i) pa (tendewa).

ii) Hubiri (tendeka)

i) Changanua sentensi hii kwa njia ya jedwali (alama 4)

Viwanda vyote vilivyoundwa juzi vitaleta faida kubwa ajabu.

j) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana za vitate: **kura** na **gura**. (alama 2)

k) Kanusha: (alama1)

Mama aliingia chumbani kisha akawapikia watoto wali.

l) Tumia kiwakilishi cha ‘a-’ unganifu katika sentensi kuonyesha: (alama 2)

i) Aina ya ii) Umilikaji m) Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari.

Ni jukumu la maskauti kupandisha bendera kila Ijumaa. (alama 2)

n) Tumia **‘o’ rejeshi ya mazoea** katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Mti ambao ulikatwa ulipelekwa uwanjani.

o) Andika katika udogo. (alama 2)

Ngamia huyo atausafirisha mzigo mzito.

p) Ainisha sentensi hii kwa kuzingatia dhamira/jukumu. (alama1)

Mezeni tembe mbili kwa maji vuguvugu kila baada ya kula.

q) Tunga sentensi iliyo na: kirai nomino, kirai kihusishi na kirai elezi. (alama 3)

u) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi: (alama 3)

Wanafunzi wataletewa zawadi bora na wazazi wao kesho kutwa.

## MTIHANI WA ISHIRINI NA SITA

**(**a) Taja vigezo viwili vya kuainisha konsonanti. (alama 2)

(b) Bainisha aina za nomino zifuatazo: (alama 2)

i) Shetani

ii) Mjombake

(c) Taja ngeli za nomino zifuatazo: (alama 2)

i) pesa ii) vita

d) Kwa kutolea mfano, eleza maana ya vitenzi elekezi. (alama 2)

e) Tambua nyakati na hali katika sentensi zifuatazo: (alama 4)

i) Rais azuru eneo la Kisumu.

ii) Wanafunzi wanafanya mtihani.

f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa – wingi. (alama 2)

Kidole cha mkono wa kushoto wa mzee huyu kimeumizwa na mlango

(g) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mchoro wa jedwali: (alama 4)

Mkongojo mrefu sana ulileta na babu utauzwa na fundi mcheshi.

h) Onyesha aina za vishazi katika sentensi ifuayo: (alama 2)

Mtihani ambao tulifanya ulikuwa mgumu sana.

(i) Andika kwa msemo wa taarifa.

**Mkutano huu utaendelea leo na kesho. Alisema mwalimu. (alama 2)**

**(j) Andika katika hali ya udogo:**

**Mbwa mwenye ukali alimfukuza mtoto .** **(alama. 2)**

k) Yakinisha. (alama 2)

**Hajui atokako wala aendako.**

(l) Tambua aina ya vitenzi.

Babu angali anasoma gazeti. (alama. 2)

m) Kwa kutungia sentensi, tofautisha vitate hivi: (alama. 2)

i) tawa ii) dawa

(n) Tumia ‗O‘ rejeshi. (alama. 2)

i) Mgeni ambaye huja ni mwanasheria.

ii) Mambo ambayo aliyasema hayasahauliki.

Mkutano huu utaendelea leo na kesho. Alisema mwalimu. (alama 2)

k) Tambua aina ya vitenzi katika sentesi hii.

Babu angali anasoma gazeti (alama. 2)

(l) Kwa kutungia sentensi, tofautisha vitate hivi. (alama. 2)

i) tawa ii) dawa

(m) Tumia ‗'O‘rejeshi. (alama. 2)

(n) Andika katika msemo wa taarifa;

(o) Kanusha sentensi hii: Mtoto huyu angalitibiwa mapema kifo kingaliepukwa.(alama. 2)

(p) Tambua shamirisho kipozi, kitondo na shamirisho ala katika sentensi ifuatayo. (alama.3)

Sikujui aliwapikia wageni chai kwa maji ya chumvi.. (alama.3)

q) Andika kinyume cha: (alama 2)

i) Dhahiri

ii) Kavu

r) Andika maana tatu zinazojitokeza katika sentensi hii: alama 3

s) Andika maana tatu zinazojitokeza katika sentensi hii: alama 3

Wengine hawahitajiki.

## MTIHANI WA ISHIRINI NA SABA

a)Fafanua vigezo vitatu vinavyotumiwa kuainisha irabu. (alama 3)

b)i)Eleza maana ya kiimbo. (alama 1)

ii)Kwa kutoa mifano miwili, eleza majukumu ya kiimbo. (alama 2)

c)Kwa kutoa mifano eleza aina mbili za mofimu. (alama 2)

d)Tunga sentensi kubainisha

i)Kihusishi cha kiwango (alama 1)

ii)Kihusishi cha a – unganifu (alama 1)

e)Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (alama 2)

i) – wa (tendea)

ii) – fa (tendesha)

f)Andika kinyume cha sentensi ifuatayo (alama 2)

Yule mama aliyeremba nyumba yake aliijika chungu jikoni.

g)Andika katika hali ya ukubwa wingi. (alama 2)

Nyoka yule alimuuma paka mguu.

h)Yakinisha sentensi hii katika nafsi ya tatu umoja. (alama 2)

Tusipoonana na wazazi hatutapata pesa.

i)Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi

Afisa wa usalama alisema kuwa wangemsaidia ikiwa angeshirikiana nao. (alama 2)

j)Bainisha vishazi katika sentensi hii.   (alama 2)

Ikiwa nitaenda nitampata mwalimu.

k)Changanua sentensi ifuatayo ukitumia njia ya matawi. (alama 4)

Simba waliojeruhiwa jana walikimbilia vichakana.

l)Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.

Alipikiwa chakula kitamu kwa jiko.  (alama 3)

m)Unda nomino mbili mbili kutokana maneno yafuatayo.   (alama 2)

i)Tepetevu

ii)Taliki

n)Akifisha

la hasha nilimpatia githeri. (alama 2)

o)Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate vifuatavyo. (alama 2)

i)Shombo

ii)Chombo

p)Andika upya sentensi ukitumia '0' – rejeshi tamati.

Gari ambalo lilianguka si lile ambalo analizungumzia. (alama 2)

q)Eleza matumizi ya ku katika sentensi ifuatayo. (alama 1)

Kulia kwake kunaudhi.

r)Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 2)

Karatasi aliyopewa na mwalimu ina dosari.

# MTIHANI WA ISHIRINI NA NANE

a) Taja sauti mbili zinazotamkiwa kwenye kaakaa laini (alama 1)

b) Eleza tofauti za sentensi zifuatazo (alama 2)
   i) Amerudi shuleni!
   ii) Amerudi shuleni.

c) Tambua aina za maneno yaliyopigiwa mstari.
   i) Afisa mkuu anafuata sharia <u>sembuse</u> wewe. (alama 1)
   ii) Ameenda huko mbali <u>sokoni</u> (alama 1)

d) Tambua aina ya vihusishi katika sentensi zifuatazo
   i) Jumba alifuatalo li mbele ya msikiti wa Musa (alama 1)
   ii) Kisiwa cha Ginigi kimekauka (alama 1)
e) Tambua hali katika sentensi ifuatayo.
   Vyungu vya aina hii vyafinyangwa na huyu. (alama 1)
f) Toa maana mbili za neno lifuatalo (alama 2)
   Somo
g) Kanusha
   Mama alimwambia sipo alime haraka
   (alama 1)
h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano
   i) Lia (Kutendeshwa) (alama 1)
   ii) -Ja (Kutendea) (alama 1)
i) Andika katika hali ya wastani umoja
   Kigombe kile kiliumia kikwato ( alama 2)
j) Akifisha sentensi ifuatayo.
   Je kuna manusura wowote yeye alitaka kujua. (alama 2)
k)
   i) Eleza maana ya kirai (alama 1)
   ii) Onyesha aina ya virai katika sentensi ifuatayo.
   Nilimpata akilalama ndani ya darasa (alama 2)
l) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi.
   Mwelekezi wake alimwambia kuwa angeweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa angeyafuata mashauri yake. (alama 2)
m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale.
   Mtoto mmoja aliyekuwa mgonjwa sana alitibiwa jana. (alama 4)
n) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia "o" rejeshi
   Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo (alama 1)
o) Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo
   Wachimba migodi wanafanya kazi haraka ipasavyo. (alama 2)
p) Tumia kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi katika sentensi (alama 2)
q) Onyesha viambishi katika fungutenzi hili ( alama 2)
   Sajilika
r) Eleza matumizi ya "na" katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
   Ndovu aliuawa <u>na</u> wawindaji haramu <u>na</u>mi nikawaripoti
s) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo ( alama 2)
i) Takrimu
ii) Sakini
t) Weka vitenzi hivi katika hali ya kuamrisha kulingana na maelezo katika mabano (alama 2)
i) -nywa (umoja)
ii) Tubu (wingi)
u) Weka neno lifuatalo katika ngeli mwafaka (alama 1)
   Nyasi

# MTIHANI WA ISHIRINI NA TISA

a) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi viwili vya silabi moja.
(alama2)

b) Onyesha sifa bainifu za sauti zifuatazo
(alama2)
   a. f/v

c) Ainisha mofimu:Awaibiaye
(alama2)

d) Eleza huku ukitoa mifano matumizi mawili ya kiambishi ‘ ji’
(alama2)

e) Huku ukionyesha upatanisho wa kisarufi weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka
(alama2)
   i. Uwele
   ii. vita

f) Tumia ‘o’ rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo
(i)Jino linauma
(ii)Jino limeng’olewa
(alama2)

g) Tambua vivumishi na uonyesha ni vya aina gani .
Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu.
(alama3)

h) Kanusha: Msichana ambaye amefika ametuzwa
(alama 1)

i) Onyesha aina za virai katika sentensi hii:
Wale wazazi wetu watawasili kesho saa tatu
(alama2)

j) Unda nomino kutokana na kitenzi ‘Haribu’
(alama1)

k) Tambua aina za vitenzi katika sentesi,
Hawa sio wachezaji waliokuwa wakicheza jana
(alama3)

l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya viunganishi vya kulinganua
(alama1)

m) Eleza matumizi mawili ya ‘ka’Toa mifano katika senstensi
(alama2)

n) Andika visawe vya maneno yafuatayo
(alama1)

i)Daawa...............................................................................................................................................

ii)
Ainisha.............................................................................................................................................

o) Jaza nafasi zilizoachwa
(alama2)

| | | |
|---|---|---|
| ____________ | Liwa | liana |
| Hoji | ________ | __________ |

p) Andika kinyume: Tajiri aliyesifiwa amelaaniwa
(alama1)

q) Changanua sentensi hii kwa kutumia vishale
Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo
(alama3)

R) Tambua vishazi na uonyeshe ni vya aina gani
Rudisha atapendwa na wengi ikiwa atashinda leo
(alama2)

s) Eleza majukumu mawili ya <u>chagizo</u> huku ukjitoa mifano
(alama2)

T) Akifisha:
Sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadillika hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote alivyorukia.
(alama3)

u) Andika ukubwa wa sentensi katika wingi: Nyundo imo dani ya kibweta
(alama1)

## MTIHANI WA THELATHINI

1. Tungia neno lifuatalo sentensi
(alama 1)
Wa'lakini
2. Taja sifa tatu za sauti ifuatayo
(alama 3)
|th|
3. Onyesha mzizi katika neno machweo
(alama 2)
4. Andika katika ukubwa
(alama 2)
Mke wa mzee huyu hupenda watoto sana.
5. Fakinisha
(alama 2)
Kama Otoyo haji mwalimu hatasahihisha kazi.
6. Tunga sentensi sahili mbili kubainisha matumizi mawilitofauti ya 'po'
(alama 2)
7. Eleza matumizi mawili ya koloni na utoe mfano kwa kutunga sentensi
(alama 2)
8. Unda nomino mbili kutokana na kitenzi kinai
(alama 2)

9. Tunga sentensi kudhihirisha ngeli ya KU-
   (alama 1)
10. Bainisha yambwa katika sentensi ifuatayo
   (alama 2)
   Askofu aliandikiwa barua na waumini
11. Bainisha virai katika sentensi
   (alama 2)
   Chake chote kilivunjika vibaya sana.
12. Changanua kwa matawi
   (alama 4)
   Ibada ya wafu iliyofanyika jana usiku ilisababisha kilio kingi.
13. Tunga sentensi moja kutofautisha ‘thibiti’ na ‘dhibiti’
   (alama 2)
14. Andika katika usemi wa taarifa
   (alama 2)
   “Aisee! yale mawimbi ya tsunami yaliangamiza biashara nyingi sana” alisema Koinange.
15.
   i) Mofimu ni nini?
   (alama 1)
   ii) Taja aina mbili za mofimu na kwa kila aina utoe mfano.
   (alama 2)
16. Andika katika hali ya mazoea kwa kutumia kirejeshi mwafaka
   (alama 2)
   Mtoto ambaye hula lishe bora ndiye hukua nyema.
17. Andika kinyume
   (alama 2)
   Wanaskauti wengi walivunja kambi jana asubuhi.
18. Tungia kitenzi kishirikishi kipungufu sentensi.
   (alama 1)
19. Tumia mzizi-enye katika sentensi kama kiwakilishi
   (alama 2)
20. Bainisha matumizi ya “ndi” katika sentensi ifuatayo.
   Tumbo lake ndilo linaloguruma
   (alama 1)

## MWISHO WA SEHEMU YA A: MASWALI. IWAPO UNAHITAJI MAJIBU YA KAZI HII NA NYINGINE NYINGI, WASILIANA NAMI KUPITIA 0707311302, MWALIMU ONYANGO. DIRA SERIES.

**MWONGOZO NI 230 KWA 0707311302, JINA LA MPESA NI JOHNSON**